



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHIRIKA LA MASOKO YA KARIAKOO**



**Barua pepe:** [info@kariakoomarket.co.tz](mailto:info@kariakoomarket.co.tz)  
**Tovuti :** [www.kariakoomarket.co.tz](http://www.kariakoomarket.co.tz)

**S.L.P 15789**  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA UMMA**

**ORODHA YA WAFANYABIASHARA WALIOHAKIKIWA 1,520 WALIOKUWEPO**  
**KABLA YA AJALI YA MOTO YA TAREHE 10.07.2021 KATIKA SOKO LA**  
**KARIAKOO**

31 Januari, 2025.

Menejimenti ya Shirika la Masoko ya Kariakoo ipo katika hatua za mwisho za kurejea kwenye shughuli zake katika Soko kuu la Kariakoo baada ya kukamilika kwa ujenzi na Ukarabati wa soko.

Ili shughuli hizo ziweze kurejea, Shirika linatangaza kwa Umma orodha ya Wafanyabiashara 1,520 ambao wamehakikiwa na Kamati iliyoungwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam. Kila mfanyabiashara atakayeona jina lake katika orodha hii, anatakiwa kufika katika Ukumbi wa **Anatoglo** kuanzia siku ya Jumatatu ya tarehe **03.02.2025 kuanzia saa 3:00 asubuhi** hadi siku ya Ijumaa ya tarehe **07.02.2025** kwa ajili ya kujisajili kwa kujaza fomu na kufuata taratibu zinginezo za kiupangaji. Mfanyabiashara anakumbushwa kufika akiwa na kitambulisho cha Taifa na namba ya Mlipakodi (TIN).

Hivyo, wafanyabiashara wenye madeni mnakumbushwa kulipa madeni yenu mnayodaiwa na Shirika ikiwa ni moja ya taratibu za kurejeshwa kabla hujapatiwa eneo la biashara.

Mwinga M. Luhoyo  
**Kny: KAIMU MENEJA MKUU**